

EWY NYONDA WANGU

1. Nyonda pokea salamu,
Hali yangu mahamumu,
Wewe kutopandwa hamu,
Ya kuja kunisalimu,
Nyonda nyuma angalia,
Uwezo andama njia.
2. Hali yangu ya mashaka,
Imesha pita miaka,
Nyonda unayo hakika
Nyonda kwa kutonifika,
Kwa hili nalalamika,
Nyonda nyuma angalia,
Upate andama njia.
3. Nyonda ingerudi jana,
Hiyo nasi kukutana,
Mengi kwako ningenena,
Jana kutokuja tena,
Kwa hili nalia sana,
Nyonda nyuma angalia,
Upate andama njia.
4. Nyonda nakuita nyonda,
Pendo ulilolipanda,
Moyoni limesha tanda,
Kwa kutochuma matanda,
Kwa hili mimi nakonda,
Nyonda nyuma angalia,
Upate andama njia.
5. Nyonda utapo jaribu,
Hata kwa dhiki na tabu,
Njoo nyonda mahabubu,
Uone yanonisibu,
Kwa hili utanitibu,
Nyonda nyuma angalia,
Upate andama njia.
6. Mimi ni kama tumbusi,
Magumu hayanighasi,
Mvumilivu kiasi,
Kingi sina wasiwasi,
Kwa hili nasema basi,
Nyonda nyuma angalia,
Upate andama njia.

(Sauti ya Kiza)
Amiri A. S Andanenga,
S.L.P 4775
Kinondoni Shamba,
Dar es Salaam